TANGAZO LA SERIKALI NA. 884 la tarehe.

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA 283)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 121)*

KANUNI ZA BIASHARA YA NYARA ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za biashara ya Nyara za Mwaka 2024.

Tafsiri

**2**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma kwa madhumuni ya Kanuni hizi.

"afisa leseni" maana yake ni afisa wanyamapori aliyeteuliwa na Mkurugenzi kuwa afisa mtoa leseni kwa madhumuni ya Kanuni hizi;

"bidhaa" maana yake ni kitu chochote kilichotengenezwa kutokana na sehemu ya nyara ambayo haijumuishi taswira za wanyamapori, ngozi nzima au kipande cha ngozi za wanyamapori iliyochakatwa au ambayo haijachakatwa;

"daktari wa mifugo" maana yake ni daktari wa mifugo wa Serikali aliyeidhinishwa na Mamlaka husika.

"eneo la kutunzia" maana yake ni eneo ambalo wanyamapori hutunzwa kwa muda kusubiri kutolewa nje ya nchi au kuingizwa kwenye maeneo ya ufugaji wanyamapori na inajumuisha eneo la kutunzia ndege, vizimba au maeneo kama hayo;

"Mkurugenzi" atakuwa na maana sawa na iliyotafsiriwa chini ya Sheria

"Kiongozi wa kimila" maana yake ni mtu ambaye anatambulika katika jamii yake kama kiongozi mkuu na kusajiliwa na Mamlaka husika;

"kituo cha karantini" maana yake ni sehemu au kituo cha kutunzia wanyamapori kwa muda kabla ya kutolewa nje ya nchi au baada ya kuwasili kutoka nje ya nchi au eneo lingine kwa lengo la ukaguzi wa afya kabla ya kuwapeleka katika maeneo ya utunzaji ili kuzuia kusambaa kwa magonjwa;

Tangazo la Serikali Na.135 la mwaka 2014

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania;

" meno machonge yaliyochomoza" maana yake ni meno ya ngiri na nguruwe pori;

"mnyamapori wa mapambo" maana yake ni mnyamapori afugwaye na kutunzwa katika nyumba za makazi, taasisi au eneo lolote ambalo wanyamapori hao watakuwa wanatunzwa;

" nyara ambayo haijaorodheshwa chini ya CITES " maana yake ni nyara ambayo haijaorodheshwa katika Mkataba wa Kimataifa wa kudhibiti Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka wa mwaka 1973;

"nyara iliyotengenezwa" maana yake ni bidhaa iliyotengenezwa kwa kutumia nyara au sehemu ya nyara.

"Nyara za Serikali" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria;

"ukamataji" maana yake ni kitendo chochote kinacholenga kuchukua mnyamapori, kiota au yai; na

Sura 283

"Sheria" maana yake Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori;

"Waziri" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## UTARATIBU WA MAOMBI NA UTOAJI WA LESENI YA BIASHARA YA NYARA

Maombi ya leseni ya biashara ya Nyara

**3**.-(1) Raia wa Jamhuri ya Muungano anayekusudia kufanya biashara ya nyara, isipokuwa kwa maombi yaliyopo chini ya kanuni ya 21, atawasilisha maombi ya Leseni ya biashara ya Nyara kwa Mkurugenzi kwa kujaza fomu na kulipa ada ya maombi kama iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi yatawasilishwa kwa Mkurugenzi yakiambatana na-

(a) nakala ya cheti cha usajili wa biashara kwa mtu ambaye anajitegemea;
(b) nakala ya cheti cha usajili wa kampuni na katiba ya mwombaji ikiwa muombaji ni mtu kwa mujibu wa sheria;
(c) nakala ya leseni ya biashara kutoka Mamlaka husika;
(d) nakala ya Namba ya Mlipa Kodi;
(e) nakala ya usajili wa kodi ya ongezeko la thamani ikiwa inahusika;
(f) nakala ya cheti cha uthibitisho wa kutodaiwa kodi; na
(g) pendekezo la mradi au mpango wa biashara unaohusiana na biashara inayopendekezwa na uthibitisho wa mtaji.

(3) Bila kujali kanuni ndogo (2), Mkurugenzi anaweza ikiwa ni muhimu na kwa madhumuni ya kuthibitisha uhalali wa nyaraka, kumtaka mwombaji kuwasilisha nakala halisi za nyaraka zilizoanishwa chini ya kanuni ndogo (2).

(4) Mkurugenzi baada ya kupokea maombi, atasajili maombi hayo na kuyafanyia uchambuzi ili kujiridhisha endapo muombaji -

(a) ana uthibitisho wa uwepo wa eneo la kutunzia wanyamapori kwa muda lililothibitishwa au maeneo mengine stahiki kwa uendeshaji wa biashara yake kwa mujibu wa CITES au mwongozo uliotolewa na Mkurugenzi; na
(b) hajawahi kutiwa hatiani chini ya Sheria

(5) Baada ya uchambuzi Mkurugenzi anaweza kukubali au kukataa maombi.

Utoaji wa leseni ya biashara ya Nyara

**4**.-(1) Endapo Mkurugenzi atakubali maombi, atamjulisha muombaji ambaye atatakiwa kulipa ada ya Leseni ya biashara ya nyara kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili ndani siku thelathini kutoka tarehe ya kujulishwa.

(2) Baada ya malipo ya ada chini ya kanuni ndogo (2), Mkurugenzi atatoa Leseni ya biashara ya nyara kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(3) Endapo maombi yatakataliwa Mkurugenzi atamjulisha muombaji sababu za kukataliwa kwa maombi yake.

(4) Mtu atakayefanya biashara ya nyara bila ya leseni ya biashara ya nyara atakuwa ametenda kosa.

Muda wa leseni ya biashara ya nyara

**5**.-(1) Leseni ya biashara ya nyara itakuwa halali kwa muda wa miaka mitatu kuanzia tarehe ya kutolewa.

(2) Leseni ya biashara ya nyara inaweza kuhuishwa baada ya muda wake kuisha kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Nne na kulipia ada ya uhuishaji kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Mbili.

(3) Maombi ya kuhuisha leseni ya biashara ya nyara chini ya kanuni ndogo ya (2) yataambatishwa na:

(a) taarifa ya utekelezaji wa biashara ya nyara kuanzia tarehe ya kutolewa kwa leseni inayomaliza muda wake hadi tarehe ya mwisho ya matumizi ya leseni hiyo; na

(b) nakala ya cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi.

Taarifa ya mabadiliko

**6**. Mmiliki wa leseni ya biashara ya nyara atamjulisha Mkurugenzi kwa maandishi kuhusu mabadiliko yoyote ya taarifa alizowasilisha wakati wa maombi ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya mabadiliko.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA LESENI NA KUFUTWA KWA LESENI YA BIASHARA YA NYARA

Masharti ya leseni ya biashara ya nyara

**7**.-(1) Mmiliki wa leseni ya biashara ya nyara atapaswa-

(a) kutokufanya biashara yoyote au kuingia kwenye mauziano yanayohusiana na aina yoyote ya nyara kinyume na Kanuni hizi;
(b) kuwasilisha kwa Mkurugenzi taarifa ya mwaka ya utekelezaji;
(c) kufanya biashara katika jengo au eneo lililoainishwa kwenye leseni au eneo lingine lolote lililoidhinishwa kwa maandishi na Mkurugenzi;
(d) kuhifadhi au kutunza nyara ndani ya eneo lililoidhinishwa na Mkurugenzi;
(e) kutenga chumba cha biashara kwa ajili ya kufanyia biashara ya nyara ikiwa jengo hilo linatumika kwa biashara nyingine, isipokuwa, sharti hili halihusiani na biashara ya nyamapori;
(f) kuweka leseni ya biashara ya nyara kwenye eneo la wazi na linaloonekana ndani ya sehemu ya jengo la biashara; na
(g) kuweka na kutunza kitabu cha kumbukumbu sahihi ya mauziano ya nyara kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tano na kukiwasilisha kwa Mkurugenzi kila robo mwaka.
(h) endapo anafanya biashara ya nyara iliyotengenezwa, kuwa na cheti cha nyara iliyotengenezwa kama ilivyo katika Jedwali la Kumi na Nne na kufanya malipo ya ada kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Mbili.

Kufuta au kusitisha leseni ya biashara ya Nyara

**8**. Mkurugenzi anaweza kufuta au kusitisha leseni ya biashara ya nyara wakati wowote kabla ya tarehe ya mwisho wa matumizi yake, endapo mmiliki wa leseni -

(a) atatoa taarifa za uongo wakati wa maombi ya leseni ya biashara ya nyara
(b) atatiwa hatiani chini ya Sheria;
(c) atashindwa kulipa ada stahiki au deni lingine lolote linalohusiana na Leseni ya biashara ya nyara;
(d) atahamisha isivyo halali kwa mtu mwingine leseni ya biashara ya nyara aliyopewa; na
(e) atashindwa kuzingatia masharti ya leseni kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Endapo Mkurugenzi atakusudia kufuta au kusitisha leseni ya biashara ya nyara atalazimika kumpa mmiliki wa leseni notisi na kumtaka kutoa sababu ndani ya siku 14, kwanini leseni hiyo isifutwe au kusitishwa

(3) Mkurugenzi anaweza, baada ya kuzingatia sababu zilizowasilishwa na mwenye leseni chini ya kanuni ndogo ya (2), kufuta au kusitisha leseni.

(4) Endapo leseni yoyote itafutwa kwa mujibu wa kanuni hii Mkurugenzi ataamuru -
(a) kutaifishwa kwa nyara; na
(b) kubatilisha nyaraka yoyote inayohusiana na nyara.

Kusalimisha leseni ya biashara ya nyara

**9**.-(1) Mmiliki wa leseni ya biashara ya nyara anaweza, wakati wowote kabla ya muda wa leseni kuisha, kuwasilisha ombi la kusalimisha leseni yake kwa maandishi kwa Mkurugenzi.

(2) Mkurugenzi, baada ya kuzingatia ombi chini ya kanuni ndogo ya (1), ataidhinisha ombi hilo kwa kuzingatia masharti yafuatayo kama Mmiliki wa leseni:
(a) amelipa ada zote anazodaiwa;
(b) amekabidhi nyaraka zote zinazoambatana na leseni;
(c) amesalimisha nyara zote zinazohusiana na leseni; na
(d) amelipa ada ya kusalimisha leseni kama ilivyoanishwa kwenye Jedwali la Kumi na mbili,

## SEHEMU YA NNE
## UINGIZAJI WA NYARA NDANI YA NCHI NA UTOAJI WA NYARA NJE YA NCHI

Uingizaji wa nyara ndani ya nchi na utoaji wa nyara nje ya nchi.

**10**.-(1) Mtu hataruhusiwa kuingiza ndani ya nchi au kutoa nyara nje ya nchi bila cheti cha kuingiza au kutoa nyara.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtu hataingiza ndani ya nchi au kutoa nyara nje ya nchi isipokuwa kwa kupitia vituo vya forodha vilivyoidhinishwa na Mamlaka husika.

Cheti cha kutoa nyara nje ya nchi

**11**. Mtu hataruhusiwa kutoa nje ya nchi nyara ambayo haijaorodheshwa chini ya CITES isipokuwa kwa cheti cha kutoa nyara nje ya nchi kutoka kwa Mkurugenzi katika fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Sita na baada ya kufanya malipo ya ada iliyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Mbili.

Masharti ya utoaji wa cheti cha kutoa nyara nje ya nchi na kuingiza nyara ndani ya nchi.

**12**.-(1) Mkurugenzi kabla ya kutoa cheti cha kutoa nyara nje ya nchi au kuingiza ndani ya nchi, atamtaka muombaji kuwasilisha nyaraka zinazoonyesha kwamba alipata nyara husika kihalali.

(2) Pale ambapo nyara mbili au zaidi zinakusudiwa kutolewa nje ya nchi au kuingizwa ndani ya nchi kama shehena moja Mkurugenzi anaweza kutoa cheti kimoja cha kuingiza au kutoa nyara nje ya nchi katika shehena hiyo.

(3) Cheti cha kutoa nyara nje ya nchi kitakuwa halali kwa muda wa siku sitini kuanzia tarehe ya kutolewa isipokuwa pale ambapo muda mrefu zaidi umebainishwa katika cheti hicho.

Kutoa nje ya nchi nyara zilizopatikana kupitia vyanzo vingine tofauti na utalii wa uwindaji.

**13**.-(1) Nyara iliyopatikana kupitia vyanzo vingine tofauti na utalii wa uwindaji haitatolewa nje ya nchi isipokuwa baada ya kulipa tofauti ya bei kati ya nyara zilizopatikana kwa vyanzo vingine na bei ya nyara zilizopatikana kwa utalii wa uwindaji.

Isipokuwa kwamba, utoaji nje ya nchi wa bidhaa zilizotengenezwa kutokana na sehemu ya nyara zitalipiwa 5% ya tofauti kati ya bei ya nyara zilizopatikana kwa vyanzo vingine tofauti na utalii wa uwindaji.

Cheti cha kuingiza nyara ndani ya nchi

**14**. Mtu hataruhusiwa kuingiza ndani ya nchi nyara ambayo haijaorodheshwa chini ya CITES isipokuwa kwa cheti cha kuingiza nyara ndani ya nchi kutoka kwa Mkurugenzi katika fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Saba na baada ya kufanya malipo ya ada iliyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Mbili

Ukaguzi wa nyara

**15**. Mkurugenzi, kabla ya kutoa cheti cha kutoa nyara nje ya nchi au kuingiza nyara ndani ya nchi, atakagua nyara iliyoombewa cheti na kujaza fomu ya ukaguzi wa nyara kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nane

Cheti cha afya cha kutoa mnyamapori hai nje ya nchi au kuingiza ndani ya nchi.

**16**.-(1) Mnyamapori hai hataingizwa ndani ya nchi au kutolewa nje ya nchi isipokuwa muombaji:

(a) amewasilisha uthibitisho kwamba, mnyamapori huyo ana afya nzuri na amepatiwa chanjo zote stahiki; na

(b) amewasilisha cheti cha afya cha mnyamapori huyo.

Kituo cha karantini

**17**.-(1) Mtu anayeingiza mnyamapori hai kutoka nje ya nchi au kutoa mnyamapori hai nje ya nchi atamuweka mnyamapori huyo kwenye kituo cha karantini akisubiri ukaguzi wa afya wa Afisa mifugo.

(2) Mnyamapori aliyeambukizwa au anayeshukiwa kuambukizwa ugonjwa atawekwa kwenye kituo cha karantini hadi Afisa mifugo atakapotoa cheti cha afya kwa mnyamapori huyo.

(3) Pale ambapo mnyamapori aliyeambukizwa na hawezi kutibiwa au kupona ndani ya miezi mitatu ataondoshwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Mifugo au kama Mkurugenzi atakavyoelekeza; na

(4) Mnyamapori hatowekwa katika kituo cha karantini kwa muda usiozidi miezi mitatu bila kibali cha maandishi cha Mkurugenzi.

Nyara iliyo safarini

**18**. Endapo nyara itasafirishwa kupitia Tanzania Bara itawasilishwa katika kituo cha forodha husika kwa ajili ya ukaguzi na kutoa idhini ya kuendelea na safari.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), kabla ya kutoa idhini ya kuendelea na safari, Mkurugenzi atajiridhisha endapo nyara hiyo ilipatikana kihalali.

(3) Endapo nyara inayosafirishwa ni mnyamapori hai na atashukiwa kuwa na ugonjwa wakati wa ukaguzi kwa kushirikiana na Mamlaka husika, itaelekezwa mmiliki kumuweka mnyamapori huyo katika kituo cha karantini kwa gharama zake mpaka atakapo ruhusiwa kuendelea na safari au kurejeshwa katika nchi alipotoka.

## SEHEMU YA TANO
## UPATIKANAJI WA NYARA KWA AJILI YA ELIMU, BURUDANI NA UTAMADUNI

Maombi ya leseni ya biasharai ya nyara kwa madhumuni ya elimu, burudani na utamaduni

**19**.-(1) Mtu anayekusudia kupata nyara kwa madhumuni ya elimu, burudani na utamaduni ataomba leseni ya biashara ya Nyara kwa Mamlaka kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Tisa na kulipa ada ya maombi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Mbili.

(2) Mkurugenzi baada ya kupokea maombi yaliyowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (1), atachambua maombi hayo na anaweza kutoa leseni ikiwa tu muombaji:

(a) ni raia wa Tanzania;

(b) amesajiliwa na kupewa leseni na Mamlaka husika

(c) amewasilisha barua ya mapendekezo kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji au Kata wa eneo analofanyia shughuli zake; na

(d) hajatiwa hatiani chini ya Sheria.

Maombi ya Nyara kwa ajili ya shughuli za elimu, burudani na utamaduni

**20**. Mmiliki wa leseni ya biashara ya Nyara chini ya kanuni ndogo ya (1), atawasilisha maombi ya nyara kwa Mamlaka kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Tisa na kulipa ada ya maombi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Mbili.

Usajili wa nyara kwa madhumuni ya elimu, burudani na utamaduni

**21**.-(1) Mkurugenzi atasajili nyara zote zilizopatikana kwa madhumuni ya elimu, burudani na utamaduni.

(2) Katika kusajili nyara chini ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi atazingatia yafuatayo:

(a) mtu huyo anamiliki leseni halali ya biashara ya Nyara;
(b) nyara hiyo ilipatikana kihalali; na
(c) mtu huyo amelipa ada husika zilizoanishwa chini ya Jedwali la Kumi na Mbili

(3) Mkurugenzi anaweza, baada ya kujiridhisha na masharti chini ya kanuni ndogo ya (2), kutoa cheti cha umiliki wa nyara kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Tatu.

Orodha ya Wanyamapori wa mapambo

**22**. Kwa muktadha wa Kanuni hii mnyamapori wa mapambo ni wale waliyoainishwa katika Jedwali la Kumi

Upatikanaji wa nyara kwa wachakata Nyara na wamilki wa maduka yanayouza Nyara zilizotengenezwa

**23**.-(1) Wachakata Nyara na wamiliki wa maduka yanayouza Nyara wanaweza kupata nyara kutoka katika vituo vya kuuza nyara vilivyoanzishwa chini ya kanuni ya 24 ikiwa:

(a) ana leseni ya biashara ya Nyara; na
(b) amelipa ada zilizoainishwa chini ya Jedwali la Kumi na Moja la Kanuni hizi.

Kuanzishwa kwa vituo vya kuuzia nyara

**24**.-(1) Mkurugenzi ataanzisha vituo vya kuuzia nyara katika maeneo anayoona yanafaa kwa madhumuni ya Kanuni hizi.

(2) Mtu anayekusudia kupata nyara kwa madhumuni ya elimu, burudani, utamaduni, kuchakata nyara, kuuza nyara zilizotengezwa au bidhaa zinazotengenezwa na nyara anaweza kununua kutoka katika vituo vilivyoanzishwa na Mamlaka.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) Mtu anaweza kununua nyara iliyotengezwa katika maduka ya nyara yaliyoanzishwa na Mamlaka.

(4) Bei ya nyara chini ya kanuni hii itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Moja.

Uhamisho wa umiliki wa nyara

**25**. Mtu hatahamisha umiliki wa nyara isipokuwa amepata kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi na kulipa ada kama ilivyoainishwa chini ya Jedwali la Kumi na Mbili.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

Upatikaji wa Nyara kwa mtu ambaye siyo raia wa Tanzania

**26**(1). Mtu ambaye siyo raia wa Tanzania anayekusudia kupata nyara atanunua kwa mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ya Nyara

(2) Mtu aliyepata nyara chini ya kanuni ndogo ya (1) na anakusudia kusafirisha nyara hizo nje ya nchi atapaswa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 12.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) mtu aliyenunua nyara kutokana na vyanzo vingine ambavyo sio uwindaji wa kitalii atalazimika kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya 13(1).

Makosa na Adhabu

**27**. Mtu anayekiuka masharti ya Kanuni hizi anatenda kosa na akitiwa hatiani, ataadhibiwa kwa kulipa faini isiyopungua milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita ama vyote kwa pamoja.

Rufaa

**28**.-(1) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mkurugenzi anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya uamuzi huo.

(2) Rufaa inayorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itakuwa kwa njia ya maandishi ikieleza sababu za rufaa hiyo.

(3) Waziri, ndani ya siku thelathini baada ya kupokea rufaa, atatoa uamuzi na kumtaarifu mrufani juu ya uamuzi uliotolewa.

Kufutwa na mpito
G.N. Na. 230 ya mwaka 2010

**29**.-(1) Kanuni za biashara ya Nyara za Mwaka 2010 zimefutwa.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), leseni, kibali, cheti au ruhusa yoyote iliyotolewa chini ya Kanuni zilizofutwa itachukuliwa kuwa imetolewa chini ya Kanuni hizi mpaka itakapoisha muda wake.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 3(1))*

FW. Na. ………

MAOMBI YA LESENI YA BIASHARA YA NYARA

| BANDIKA PICHA HAPA |
|---|

1. Jina kamili la muombaji/Kampuni……………………………………………...……………
2. Jinsia………………………………………. 3. Umri ………………………
4. Uraia ……………………………………… 5. Anuani ya makazi…………
6. Anuani ya biashara
(i) S.LP…………………………...(ii) Simu ya mkononi……….………………..
(iii) Barua pepe ……………...…. (iv) Namba ya kiwanja..……..………………
(v) Mtaa/Eneo………………… ……(vi) Mji/Mahali ….…………………………..
(vii) Msimbo wa posta………………
(viii) Nukushi……………………….

7. Daraja la leseni ya biashara ya Nyara linaloombwa…………..………………………………
8. Ukubwa wa (i) Kiwanda (m²)…………………………..… (ii) Chumba cha maonesho ya nyara na bidhaa zinazotokana na nyara (m²)……………….………………………………………
(iii) Eneo la kutunzia wanyamapori kwa muda (hekta) …………………….(iv) Kituo cha kutunzia wanyamapori kwa ajili ya uangalizi wa afya (hekta) ……………
(v) Eneo la kufugia wanyamapori (hekta)…………………………………………

9. Idadi ya viwanda ……../chumba cha maonesho ya nyara na bidhaa zinazotokana na nyara……./stoo……../ Ghala……./ Eneo la kutunzia wanyamapori kwa muda……/ Kituo cha kutunzia wanyamapori kwa ajili ya uangalizi wa afya….…/ Eneo la kufugia wanyamapori…… / matawi (ikiwa yapo)

10. Ikiwa ni kiwanda au duka kuu elezea kwa kina kuhusu matawi yake …………………………

……………………………………………………………………………………………………..
11. Chanzo cha nyara ……………………………..……………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………….
12. Aina nyingine ya biashara inayofanyika katika kiwanda /duka ……………………………….

…………………………………………………………………………………………………….
13. Kiwango cha mtaji utakaowekezwa kama ilivyoainishwa katika andiko la biashara………

*Tangazo la Serikali Na.884 (Linaendelea.)*

14. Je, umeshawahi kunyimwa leseni ya biashara ya Nyara nchini Tanzania, au nchi nyingine?....................................................ikiwa ndiyo, eleza sababu…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

15. Je, umeshawahi kufutiwa leseni uliyopatiwa chini ya Sheria ya sasa au Sheria iliyofutwa ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Tanzania au Sheria ya Wanyamapori ya nchi nyingine?................. Ikiwa ndiyo, Eleza sababu………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………

16. Je, umeshawahi kutiwa hatiani kwa kosa kinyume na Sheria ya sasa au Sheria iliyofutwa ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Tanzania au Sheria ya Wanyamapori ya nchi nyingine?.............. Ikiwa ndiyo, Eleza aina ya kosa/makosa……………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

TAMKO

Mimi …………………………………………………………. ninathibitisha kuwa taarifa nilizozitoa hapo juu ni sahihi na nimezitoa nikiwa na akili timamu na ninafahamu matakwa ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura 283.

……………………………………. ……………………………………

*Saini ya mwombaji* *Tarehe*

<u>KWA MATUMIZI YA OFISI TU</u>

MAPENDEKEZO:

**1)** Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya
………………………………………………………………………
………………………………………………………………………
………………………………………………………………………
………………………………………………………………………
………………………………………………………………………
………………………………………………………………………

…………………………………… …………………………

*Saini na muhuri*

Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya *Tarehe*

MAAMUZI YA MKURUGENZI

Maombi haya;

1) Yamekubaliwa …………………………………..………….
2) Yamekataliwa………………………………………………..

…………………………………….. …….. ……………………………………..

Saini ya Mkurugenzi Tarehe

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

ADA YA MADARAJA YA LESENI YA BIASHARA YA NYARA

| Daraja la leseni | Maelezo | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Kushughulika na Biashara ya meno mazima ya kiboko au meno ya ngiri au vipande ambavyo havijachakatwa zaidi ya kuandaliwa kwa ajili ya kuhifadhiwa. | 450,000 |
| 2 | Kushughulika na Biashara ya ngozi nzima za wanyamapori au vipande vya ngozi ambazo hazijachakatwa zaidi ya kuandaliwa kwa ajili ya kuhifadhiwa. | 300,000 |
| 3 | Kung'arisha, kuchonga, kutengeneza au kuchakata kibiashara meno ya kiboko au meno ya ngiri na kuuza meno hayo au bidhaa inayotokana na meno hayo. | 300,000 |
| 4 | Kukata, kutengeneza au kuchakata kibiashara ngozi zilizotengenezwa za chui, simba, mondo, au ngozi za paka wengine na kushughulika na bidhaa zinazotokana na ngozi hizo. | 450,000 |
| 5 | Kukata, kutengeneza au kuchakata kibiashara ngozi zilizotengenezwa za wanyamapori na kushughulika na bidhaa zinazotokana na ngozi hizo. | 300,000 |
| 6 | Biashara ya nyara zilizotengenezwa. | 300,000 |
| 7 | Kusindika, kuweka kemikali za kuondoa manyoya ngozi za wanyamapori. | 600,000 |
| 8 | Kuchakata kibiashara au kushughulika na mifupa ya wanyamapori, pembe au miguu na bidhaa zinazotokana na nyara hizo. | 300,000 |
| 9 | Kuchakata kibiashara au kushughulika na mikia ya wanyamapori isipokuwa mikia ya tembo na faru na bidhaa zinazotokana na mikia hiyo. | 300,000 |
| 10 | Huduma ya ugomboaji na uondoshaji wa nyara. | 600,000 |
| 11 | Kushughulika na biashara ya ndege hai au waliokaushwa. | 450,000 |
| 12 | Kushughulika na biashara ya wanyamapori hai jamii ya nyani. | 450,000 |
| 13 | Kushughulika na biashara ya mamalia hai isipokuwa wanyamapori jamii ya nyani. | 600,000 |
| 14 | Kushughulika na biashara ya wanyamapori hai jamii ya mijusi au waliokaushwa. | 450,000 |
| 15 | Kushughulika na biashara ya wanyamapori hai wengine au waliokaushwa. | 450,000 |
| 16 | Bustani ya wanyamapori. | 600,000 |
| 17 | Shamba la ufugaji wa wanyamapori. | 900,000 |
| 18 | Ranchi ya wanyamapori iliyo wazi. | 900,000 |
| 19 | Ranchi ya wanyamapori yenye uzio. | 1,200,000 |
| 20 | Kituo cha uangalizi wa afya ya wanyamapori. | 600,000 |
| 21 | Eneo la kutunzia wanyamapori kwa muda maalum. | 300,000 |
| 22 | Eneo la kufugia wanyamapori walio hatarini kutoweka. | 900,000 |
| 23 | Eneo la kuzalisha wanyamapori. | 900,000 |
| 24 | Eneo la matumizi mseto. | 900,000 |
| 25 | Kituo cha kuuza nyamapori. | 900,000 |
| 26 | Kushughulika na wanyamapori hai au Nyara nyingine kwa ajili ya shughuli za elimu, burudani na utamaduni | 300,000 |

*Tangazo la Serikali Na.884 (Linaendelea.)*

| Daraja la leseni | Maelezo | Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 27 | Biashara ya Nyara kwa ajili shughuli ya kiongozi wa mila | 90,000 |
| 28 | Kituo cha kulelea wanyamapori yatima. | 300,000 |
| 29 | Kushughulika na biashara nyingine ya nyara zaidi ya zilizoainishwa katika daraja la (1) hadi daraja la (28) hapo juu kama itakavyoainishwa katika leseni. | 300,000 |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2))*

FW. Na……

LESENI YA BIASHARA YA NYARA

HALISI (HAIHAMISHIKI)

Namba ya Leseni………………………………………………………………………..

Mahali ilipotolewa …………………………………………………………………………

Tarehe ya kutolewa ……………………………………………………………………..........

Tarehe ya Mwisho ya Matumizi ……………………………………………………………

Jina kamili la mfanyabiashara ………………………………………………………………

Anuani ya biashara:

S.L.P ……………………………… Simu ya mezani……….………………..

Baruapepe ……………….………...Namba ya kiwanja… …………..……

Mtaa/Eneo ………………… .Mji/Eneo ….……………Nukushi……...…….

Daraja la leseni na maelezo ya biashara……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

Ada iliyolipwa kwa maneno ………………………………………………………...........

(Tsh:………………………………………………………………………………………)

……………………………………… ………………………………………………..

Saini ya mwenye leseni Saini ya afisa mtoa leseni na muhuri wa ofisi

Terehe: ……………………………… Tarehe: …………………………………

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 5(2)*

FW.Na………

FOMU YA MAOMBI YA KUHUISHA LESENI YA BIASHARA YA NYARA

BANDIKA PICHA HAPA

1. Jina kamili la muombaji/kampuni
……………………………………………...……………
2. Jinsia…………………………………………… 3. Umri……………………………
4. Uraia ……………………………………………. 5. Anuani ya makazi ……………
6. Anuani ya biashara
(i) S.L.P ……………………………...(ii) Telephone(s)………….……………
(iii) Barua pepe ……………………..…(iv) Namba ya kiwanja. …………..……
(v) Mtaa/Eneo………………………. ..(vi) Mji/Mahali……. …..…………………

7. Daraja la leseni ya biashara ya nyara inayohuishwa……………………..……………………
8. Namba ya leseni ya awali…………………………..mahali ilipotolewa………….………Tarehe ya kutolewa …………………………..…………tarehe ya mwisho ya matumizi………………

9. Aina nyingine ya biashara inayofanyika katika kiwanda/duka……………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

10. Je, umeshawahi kupatiwa leseni ya biashara ya Nyara chini ya Sheria ya sasa au Sheria iliyofutwa ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Tanzania au Sheria ya Wanyamapori ya nchi nyingine ambayo ilisitishwa au kufutwa?......................................... Ikiwa ndiyo, toa sababu……………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
11. Je, umeshawahi kutiwa hatiani kwa kosa kinyume na Sheria ya sasa au Sheria iliyofutwa ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Tanzania au Sheria ya Wanyamapori ya nchi nyingine?………………………………Ikiwa ndiyo, Eleza aina ya kosa/makosa………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

TAMKO

Mimi ………………………………………………………. ninathibitisha kuwa taarifa nilizozitoa hapo juu ni sahihi na nimezitoa nikiwa na akili timamu na ninafahamu matakwa ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura 283.

…………………………………………….. …………………………………………………

*Saini ya mwombaji* Tarehe

<u>KWA MATUMIZI YA OFISI TU</u>

MAPENDEKEZO:

**1)** Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya

……………………………………………………………………
……………………………………………………………………
……………………………………………………………………
……………………………………………………………………
……………………………………………………………………
……………………………………………………………………
…………………………………………………

……………………………………. ……………………………

*Saini na muhuri wa*
*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya* *Tarehe*

MAAMUZI YA MKURUGENZI

Maombi haya:

Yamekubaliwa ……………………………………………………….
Yamekataliwa …………………………………………………………..

………………………………… ……………………………………..

*Saini ya Mkurugenzi* Tarehe

______________

JEDWALI LA TANO

________________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 7(1)(g)*

FW.Na……….

FOMU YA USAJILI WA NYARA KWA WABIASHARA YA NYARA

Aina ya nyara au bidhaa iliyotengenezwa…………………………………………………………….
Imetoka ukurasa wa……………………………………………………………………………….
Namba ya ukurasa………………………………………………………………………………………

| Na | Jina la mnyama | Tarehe | Aina ya Nyara | Mahali nyara ilipopatikana | Namba ya kibali | Namba ya Cheti ya kumiliki nyara | Namba ya Cheti ya kumiliki nyara zilizotengenezwa | Idadi | | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | zilizopokelewa | Zilizouzwa | Zilizosalia | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | |

Jina la mkaguzi…………………………… Saini …………………………..Tarehe…………………

## JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni (11))*

FW.Na. ………

| JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA<br>CHETI CHA UTOAJI NYARA /KURUDIA KUTOA NYARA NJE YA NCHI<br>HALISI (HAIHAMISHIKI)<br>Na……………. | |
|---|---|
| Imetolewa kwa …………………………<br>wa (anuani)<br>…………………………………<br>……………………………………………<br>… | Tarehe ya kutolewa………………………………<br>Tarehe ya mwisho ya matumizi………………… |
| Hii ni idhini ya utoaji/kurudia utoaji Nyara zilizoainishwa hapa chini kwenda kwa……………………………………<br>……………………………………………<br>………..……………………………………<br>…………..<br>(Jina na anuani) | Kwa madhumuni ya:<br>………....................................<br>……………………………………………………<br>……………………………………………………<br>……………………………………………………<br>…………………………………………………… |

| Na. | Aina ya Nyara | Idadi | Uzito (Kg) | Daraja | Alama ya Usajili | Cheti au Idhini nyingine | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Aina | Namba | Mahali | Tarehe |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

| Kny:Mkurugenzi |
|---|
| ……………………………………………….. |

| Angalizo |
|---|
| 1. Uhalali wa matumizi ya Cheti hiki hautazidi siku 60 tangu tarehe ya kutolewa.<br>2. Cheti hiki lazima kiambatane na Nyara zilizoainishwa hapo juu kwa muda wote mpaka nyara zitakapomfikia mmiliki.<br>3. Ikiwa Nyara zinapotakiwa kutolewa nje ya nchi zinalindwa na Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo Hatarini Kutoweka kibali cha utoaji Nyara nje ya nchi lazima kitolewe na Mkurugenzi |

JEDWALI LA SABA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 14)*

FW. Na……….

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

CHETI CHA KUINGIZA NYARA NCHINI

HALISI (HAIHAMISHIKI)

Na………………….

| | |
|---|---|
| Imetolewa kwa ………………………………<br>wa (anuani)……………………………………. | Tarehe ya kutolewa…………………………<br>Tarehe ya mwisho kutumika……………… |
| Hii ni idhini ya kuingiza Nyara zilizoorodheshwa hapa chini<br>…………………………………………………<br>…………………………………………………<br>(jina na anuani) | Kwa madhumuni ya:<br>……………………………………………<br>………………………………………………<br>………………………………………………<br>………………………………………………<br>……………………………………………… |

| Na | Aina ya nyara | Idadi | Uzito (kg) | Daraja | Alama ya usajili | au idhini nyingine | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Aina | Namba | Mahali | Tarehe |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

| Saini ya msafirishaji | Tarehe na muhuri wa afisa muidhinishaji | Mkurugenzi |
|---|---|---|
| ………………………… ………………. | …………/…………/………. | ………………………………… ……………….. |

| Angalizo |
|---|
| 1. Uhalali wa matumizi ya cheti hiki hautazidi mwaka mmoja tangu tarehe ya kutolewa.<br>2. Cheti hiki lazima kiambatishwe na Nyara zilizoainishwa hapo juu kwa muda wote mpaka Nyara zitakapomfikia mwingizaji/mmiliki.<br>3. Ikiwa Nyara zinapotakiwa kuingizwa nchini zinalindwa na Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo Hatarini Kutoweka kibali cha kuingiza nyara nchini lazima kitolewe na Mkurugenzi |

______________

JEDWALI LA SABA

_________________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 14)*

FW. Na……….

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

CHETI CHA KUINGIZA NYARA NCHINI

HALISI (HAIHAMISHIKI)

Na………………….

| | |
|---|---|
| Imetolewa kwa ………………………………<br><br>wa<br>(anuani)………………………………………. | Tarehe ya kutolewa…………………………<br><br>Tarehe ya mwisho kutumika……………… |
| Hii ni idhini ya kuingiza Nyara zilizoorodheshwa hapa chini<br>…………………………………………………<br>…………………………………………………<br>(jina na anuani) | Kwa madhumuni ya:<br>……………………………………………<br>………………………………………………<br>………………………………………………<br>………………………………………………<br>……………………………………………… |

| Na | Aina ya nyara | Idadi | Uzito (kg) | Daraja | Alama ya usajili | au idhini nyingine | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Aina | Namba | Mahali | Tarehe |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

| Saini ya msafirishaji | Tarehe na muhuri wa afisa muidhinishaji | Mkurugenzi |
|---|---|---|
| ………………………………<br>…………. | …………/…………./<br>……….. | ……………………………………<br>…………….. |

| Angalizo |
|---|
